



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA MAJI USHIROMBO

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa mamlaka ya Maji)

WIZARA YA MAJI



MKATABA WA UCHIMBAJI WA MITARO YA MABOMBA

MKATABA NA.LGA.113/2022/2023/MJ/.....02

MKATABA WA UCHIMBAJI WA MITARO YA MABOMBA

KATI YA

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA USHIROMBO (UWSSA) SLP 02
BUKOMBE (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “Mwajiri”) kwa upande
mmoja,

NA

MICHAEL ZEPHANIA (LOCAL FUNDI) WA SLP 02 USHIROMBO (ambaye katika
mkataba huu atajulikana kama “Mwajiriwa”) kwa upande mwingine.

KWA KUWA: Mwajiri anayo kazi ambayo amehiyari na anayo nia ifanywe na
mwajiriwa, kazi ya kuchimba mitaro kwa ajili ya ulazaji wa mabomba.

NA KWA KUWA: Mwajiriwa yuko tayari na anao uwezo wa kuchimba mitaro kwa
ajili ya ulazaji wa mabomba.

HIVYO BASI MKATABA huu ni ushuhuda wa makubaliano **kwamba:**

1. Mwajiriwa anao uwezo wa kufanya kazi ya uchimbaji wa mitaro na kazi hiyo atatakiwa kuifanya kwa kuzingatia viwango na ubora unaotakiwa, na hili litakuwa sharti la msingi la mkataba huu.
2. Msimamizi wa kazi hii ni Mhandisi wa maji RUWASA Bukombe ambaye atatoa maelekezo ya kazi, atasimamia, atakagua na kutoa taarifa ya ubora wa kazi kwa Mwajiri.
3. Mwajiri atapaswa kumlipa Mwajiriwa kiasi cha **Tsh 4,042,600/=**
4. **Kwamba**, Mwajiriwa atabidhiwa kazi ya uchimbaji wa mitaro mita **2,065** ambapo kila mita itachimbwa kwa **Tsh1, 000** na mitaro hiyo itachimbwa mtaa wa kapela kata ya Igulwa.
5. **Kwamba**, Mwajiriwa atakabidhiwa kazi ya uchimbaji wa mitaro mita **1,523** Ambapo kila mita itachimbwa kwa **Tsh 1,200** na mitaro hiyo itachimbwa mtaa wa Muungano Kata ya Bulangwa.
6. **Kwamba**, Mwajiriwa atafanya kazi ya kuchimba mitaro ya mabomba kwa kuzingatia “specifications” za uchimbaji ambazo ni kina cha urefu wa sentimita 75.
7. **Kwamba**, Mwajiriwa atabeba mabomba nnchi 3 roller 14,nnchi 2 roller 12 na 1 ½ roller 02 kutoka ofisi ya Mamlaka ya maji ushirombo kupeleka site kwa shilingi laki moja na nusu (**Tsh 150,000/=**)
8. **Kwamba**, Mwajiriwa atafukia bomba baada ya Fundi bomba kukamilisha ufungaji na ulazaji wa mabomba.
9. Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote kati ya Mwajiri na Mwajiriwa, mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya usuluhishi utakao simamiwa na Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe na endapo usuluhishi utashindwa kufikia muafaka, basi mgogoro huo utaelekezwa katika vyombo vya sheria (Mahakama) na maamuzi yatakayotolewa na Mahakama yatakuwa ya mwisho.

10. Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku¹⁴..... za kwenye kalenda bila kuondoa siku za sikukuu na mapumziko, kuanzia tarehe ...^{2/7/2022} hadi tarehe ^{15/7/2022}.....

11. Mkataba huu unaweza kusitishwa na upande wowote wa mkataba kwa kutoa taarifa ya siku saba (7) kwa maandishi inayoeleza sababu za msingi za kusitisha mkataba huu.

Pande zote mbili zimekubaliana na kutia saina kwenye makubaliano haya na ni wazi kuwa kila upande umesoma na kuelewa vipengele vyote vya mkataba huu, na kutia saina leo tarehe ^{2/7}.....mwezi.....⁰⁷.....2022.

UMETOLEWA (MWAJIRI)

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji,
Jina kamili.....^{SCHOLA E. NDONYO}.....
Saini.....^[Signature].....
Tarehe.....^{2/7/2022}.....

Mhuri wa ofisi.....
**KNY. MKURUGENZI MTENDAJI
MAMLAKA YA MAJI SAPI NA USABU
WA MAZINGIRA USHIRUMBU
S. L. P. 02
BUKOMBE**

Umesainiwa na kupokelewa (Mwajiriwa)

Jina Kamili.....^{MALCO ZEPHURIA}.....
Saini.....^[Signature].....
Tarehe.....^{2/7/2022}.....
Wadhifa.....^{R.O.C.A.L.FUNDI}.....

Mwenyekiti wa Bodi wa mamlaka ya maji

Jina kamili.....^{PETER DAVID}.....
Saini.....^[Signature].....
Tarehe.....^{02/07/2022}.....

Shuhuda wa Mwajiriwa

Jina Kamili.....^{LAURENT MAHEE}.....
Saini.....^[Signature].....
Tarehe.....^{2/7/2022}.....
Wadhifa.....

MHURI WA MWANA SHERIA WA HALIMASHAURI.

JINA KAMILI.....^{Daniel}.....
CHEO.....^{S.A}.....SAHIHI.....
TAREHE.....^{02/07/2022}.....

